

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 1 Biblia

Maswali na Majibu

1. Vitabu vingapi viko kwa Biblia?
Vitabu 66 – vitabu 39 kwa Agano la Kale na vitabu 27 kwa Agano Jipya.
2. Neno 'Agano' lina maana gani?
Ni mapatano. Biblia ni mapatano kati ya Mungu na wanadamu
3. Vitabu vya aina gani viko kwa Agano la Kale?
Sheria, historia, Zaburi za kuimba, misemo ya hekima na manabii
4. Vitabu vya aina gani viko kwa Agano Jipya?
Injili 4 – maisha ya Yesu, Matendo – inayohubiri Injili, barua, unabii.
5. Agano la Kale iliandikwa kwa lugha gani? *Kiebrania*
6. Agano Jipya iliandikwa kwa lugha gani? *Kiyunani*
7. 'Upuzio' ni nini?
Mungu aliongoza watu walioandika Biblia kwa kuwapa ujumbe wake.
8. Ujumbe wa Mungu kwa Biblia una twambia nini?
Vile Mungu anataka sisi tuishi. Juu ya Ufalme wake waajabu utakaokuja hapa duniani.

Mistari ya kukariri

Jifunze vitabu vya Biblia pole pole kwa majuma machache yajayo.

Mazungumzo

Tafuta mistari ifwatayo. Inatufundisha nini juu ya vile Biblia imeandikwa?

2 Samweli 23:2; Jeremia 36 mistari 1-2, 27 & 32; Yohana 14:26

2 Petro 1:21; 2 Timotheo 3:16 – 17; Warumi 15:4

Kuandika

Chagua kitabu kimoja kutoka kwa Biblia na uandike muhtasari mfupi juu yake.

SOMA 2 Timotheo 3:16—17 & Warumi 15:4

SOMO

Neno 'Biblia' linamaanisha 'Kitabu'. Biblia siku zote imeitwa Biblia takatifu kwa sababu ni kitabu cha kipekee. Ni ujumbe kutoka kwa Mungu. Biblia inazungumza juu ya Mungu na kusudi lake kwa wanadamu.

Biblia ina sehemu nyingi zilizosanywa pamoja na kuwa kitabu kimoja kikubwa. Kila sehemu inaitwa kitabu. Kila kitabu kimetengwa kando na kina mwandishi tofauti na kiliandikwa wakati wake. Biblia nzima ina vitabu 66. Kwa hivyo Biblia ni kama maktaba ya vitabu.

AGANO LA KALE INA VITABU 39	AGANO JIPYA INA VITABU 27
------------------------------------	--------------------------------------

Hivi vitabu vimegawanywa kwa sehemu mbili na zinaitwa agano. Kuna Agano la Kale na Agano Jipya. Agano lina maana ya 'ahadi' au 'mapatano'. Biblia inatwambia mapatano kati ya Mungu na wanadamu – mapatano ya zamani na mapatano mapya. Angalia mwanzo wa Biblia yako. Utaona orodha ya majina ya vitabu vyote. Hii ni ya kukusaidia upate kitabu chochote unachotaka kuangalia. Ni vizuri kushika orodha ya hivi vitabu moyoni. Jaribu kama unaweza kufanya hivyo kwa majuma machache yajayo.

Kila kitabu kimegawanywa kwa milango, na kila mlango umegawanywa kwa mistari. Kwa hivyo ukiulizwa kutafuta mahali popote kutoka kwa Biblia, utaambiwa kitabu, mlango halafu mistari. Kwa mfano: Kitabu cha Isaya, mlango wa 2, mistari wa 4. Itafupishwa namna hii – Isaya 2:4. Hebu tafuta huo mistari na usome.

Vitabu vya Agano la Kale viliandikwa zamani sana na kwa muda mrefu. Vitabu vya kwanza viliandikwa miaka 1,400 kabla ya Yesu (BC). Kitabu cha mwisho kiliandikwa karibu miaka 400 kabla ya Yesu. Kwa hivyo Agano la Kale iliandikwa kwa saidi ya muda wa miaka elfu moja. Agano Jipya iliandikwa kwa chini ya muda wa miaka 40. Kitabu cha kwanza kiliandikwa karibu miaka 50 baada ya kuzaliwa kwa Yesu (AD) na cha mwisho kiliandikwa sio saidi ya miaka 90 baada ya Yesu.

Katika Agano la Kale kuna vitabu vya Sheria za mafundisho ya Mungu, vitabu vya historia, vitabu vya Zaburi za kuimba na misemo za hekima. Kuna maneno ya manabii – watu walioleta ujumbe kutoka kwa Mungu wakisema matokeo yatayokuweko. Katika Agano Jipya kuna habari za Injili nne – zinazungumzia maisha ya Yesu na mafundisho yake. Kuna historia ya mahubiri ya wafwasi wa Yesu. Kuna barua zilizoandikiwa makanisa ya Wakristo wa kwanza. Kitabu cha mwisho ni kitabu cha unabii kikiangazia mambo yajayo.

Miaka mingi iliyopita vitabu viliandikwa kwa chuo cha ngozi kutoka kwa wanyama na kutengenezwa vizuri. Baadaye viliandikwa kutoka kwa manyasi iliyoonekana kama karatasi. Hizi chuo zilikuwa vipande vya ngozi au manyasi. Viliandikwa kwa sehemu. Zilifiringiswa kwa fito viwili vifupi. Zilifiringiswa zikielekeswa nyuma au mbele kutafuta sehemu inayo hitajika kuandika au kusoma.

Agano la Kale iliandikwa kwa lugha ya Kiebrania. Agano Jipya iliandikwa kwa lugha ya Kiyunani. Kabla ya uvumbuzi wa kupika chapa, nakala mpya ziliandikwa kwa mkono. Nakala moja ilichukuwa muda mrefu kutengeneza. Baadaye nakala zilizoandikwa kwa mkono zilitolewa kama vitabu.



Biblia mzee iliyoandikwa kwa mkono



Biblia imetafsiriwa kutoka kwa Kiebrania na Kiyunani na kuandika kwa lugha zingine nyingi. Tunaziita ‘tafsiri’ za Biblia.

Karibu miaka 500 zilizopita Biblia imetafsiriwa kwa Kingereza. Tafsiri inayojulikana sana ni Biblia Iliyohalalishwa. Tafsiri iliyo Halaliswa - Authorised Version. Imetumiwa kutoka wakati huo mpaka saa hii. Wakati mwingine hii Biblia (AV) ni ngumu kuelewa. Kwa huu muda wa miaka 500, lugha ya Kingereza imebadilika. Maana ya maneno mengine imebadilika.

Tafsiri za Biblia zimeandikwa kwa Kingereza cha sasa. Labda unaweza kuwa una moja yake. Zingine zinatafsiri nzuri kuliko zingine. Hata labda unaweza kuwa una moja yenye imetafsiriwa kwa lugha yako.

Kumbuka kwamba ujumbe na mafundisho ya Biblia kawaida huwa sawa. Lugha yenye inanakiliwa na kutasafiriwa kwa imani haitakiwi kubadilisha maana ya ujumbe.

Biblia ni tofauti na ni ya kipekee. Watu walioandika Biblia, hawakuandika maneno yao tu. Waliandika vile walikuwa wakiongozwa na Mungu. Tunaita huu uongozi ‘upuzio’. Mungu ndiye aliwapa watu hao ujumbe na wakaandika chini hayo mawazo na maneno kutoka kwa Mungu.

Mungu alijitaabisha sana kutuletea huu ujumbe katika Biblia. Wakati mwingine watu waovu wamejaribu kuharibu maneno ya Mungu yaliyomo kwa Biblia. Lakini Mungu amewezesha mpaka Biblia imezidi kukaa. Leo hii Biblia imetafsiriwa kwa mamia ya lugha nyingi. Tunaweza kusoma neno la Mungu kwa lugha zetu.

Biblia ni ujumbe wa Mungu kwako. Inatwambia vile Mungu anataka tuishi. Inatupa tumaini la kuishi milele katika Ufalme wa Mungu utakaosimamishwa hapa duniani.